

# JICHUNGE!

**Kipimo kinatoa ufafanuzi kuhusu afya yako**

Una maswali yoyote kuhusu afya yako ya ngono? Unataka kujifunza kuhusu VVU (HIV) na UKIMWI? Tunaweza kukusaidia.

Leo, magonjwa yanaweza kutibiwa vizuri au hata kuangamizwa. Ambukizo la VVU haimaanishi kuwa utakuwa na UKIMWI au kuaga dunia. Kuna njia moja pekee ya kujua ikiwa umeambukizwa VVU: Nenda upimwe.

Endapo utapatikana na VVU, njia bora za matibabu zinazopatikana leo zinamanisha kuwa huenda ukaishi maisha ya kawaida na yenye afya na kuzaa watoto wenye afya. Na ikiwa unajua hali yako, hutataka kuwaambukiza wengine.

## MAMBO MUHIMU YA KUJUA:

Ambukizo la VVU ambalo halijatibiwa linaweza kusababisha UKIMWI, unaoweza kusababisha kifo.

Huwezi kufahamu ikiwa una VVU au huna! Havionekani. Watu walio na VVU mara nyingi hawaonekani kuwa wagonjwa.

Mtu yeyote (bila kujali nchi asili, umri, jinsia au mvuto wa jinsia) anaweza kuambukizwa!

## JINSI VVU VINAVYOWEZA KUAMBUKIZWA:

Mapenzi yasiyo ya kinga na mwanamke au mwanamume. Mpira huzuia VVU na maambukizi mengine ya magonjwa ya zinaa (STIs).

Matumizi yanayoshirikiwa ya sindano ambazo zimegusa damu ya mtu (kama inavyofanyika wakati mwingine kwa matumizi ya dawa).

Ikiwa mama ana VVU na hatumii dawa zozote za VVU, VVU vinaweza kusambazwa kwa mtoto (wakati wa kujifungua au wakati wa kunyonyesha).

## VVU HAVIWEZI KUSAMBAZWA:

Kwa kukaa karibu na watu wenye VVU (nyumbani, kazini, kwenye garimoshi...)

Kula au kunywa kwa kutumia vyombo sawa.

Kubusu, kupapasa, au kupiga pambaja.

Imechapishwa na: AIDS-Hilfe Potsdam
Wir fördern Gesundheit.

## USHAURI NASAHA NA VIPIMO VYA BILA MALIPO: WAPI?

**Brandenburg (Havel)**

**OFISI YA DAKTARI**
Klosterstraße 14
14770 Brandenburg
an der Havel
**T +49 3381 585320**

**Cottbus**

**UKUMBI WA JIJI COTTBUS**
Puschkinpromenade 25
03044 Cottbus
**T +49 355 6132215**

**BÜNDNIS FAIRES BRANDENBURG E.V.**
Rat- und Tatzentrum
Cottbus
Straße der Jugend 33
03050 Cottbus
**T +49 321 21335991**

**Frankfurt (Oder)**

**OFISI YA DAKTARI**
Logenstraße 6
15230 Frankfurt (O)
**T +49 335 5525313**

**Potsdam**

**UKUMBI WA JIJI POTSDAM**
Ofisi ya Daktari,
Room 505
Jägerallee 2
14469 Potsdam
**T +49 2892434/-2412**

**Landkreis Barnim**

**OFISI YA DAKTARI**
Am Markt 1
16225 Eberswalde
**T +49 3334 2141601**

**Landkreis Dahme-Spreewald**

**KITUO CHA USHAURI KUHUSU UKIMWI**
Beethovenweg 14
15907 Lübben
**T +49 3546 201784**

**KITUO CHA USHAURI KUHUSU UKIMWI**
Schulweg 1B
15711 Königs Wusterhausen
**T +49 3375 263019**

**Landkreis Elbe-Elster**

**OFISI YA DAKTARI**
Grochwitzer Straße 20
04916 Herzberg
**T +49 3535 463108**

**Landkreis Havelland**

**OFISI YA DAKTARI**
Forststraße 45, House A
14712 Rathenow
**T +49 3385 5517110**

**OFISI YA DAKTARI**
Goethestraße 59/60
14641 Nauen
**T +49 3321 4035306**

**OFISI YA DAKTARI**
Dallgowerstr. 9
14312 Falkensee
**T +49 3321 4036820**

**Landkreis Märkisch-Oderland**

**OFISI YA DAKTARI**
Klosterstraße 14
15344 Strausberg
**T +49 3346 850 6710/-6711**

**Landkreis Oberhavel**

**OFISI YA DAKTARI**
Havelstr. 29
16515 Oranienburg
**T +49 3301 601 3781/-3773**

**Landkreis Oberspreewald-Lausitz**

**OFISI YA DAKTARI**
Großenhainer Straße 62
01968 Senftenberg
**T +49 3573 8704326/-4322**

**Landkreis Oder-Spree**

**OFISI YA DAKTARI**
Am Bahnhof 1, House 1
15517 Fürstenwalde
**T +49 3361 35 2213**

**OFISI YA DAKTARI**
Brandstr. 39
15848 Beeskow
**T +49 03366-35 2213**

**Landkreis Ostprignitz-Ruppin**

**OFISI YA DAKTARI**
Neustädter Straße 44
16816 Neuruppin
**T +49 3391 6885366**

**Landkreis Potsdam-Mittelmark**

**OFISI YA DAKTARI**
Steinstraße 14, Room 104
14806 Bad Belzig
**T +49 33841 91306**

**OFISI YA DAKTARI**
Lankeweg 4
14513 Teltow
**T +49 3328 318135**

**Landkreis Prignitz**

**OFISI YA DAKTARI**
Bergstraße 1
19348 Perleberg
**T +49 3876 713549**

**Landkreis Spree-Neiße**

**OFISI YA DAKTARI**
Heinrich-Heine-Straße 1
03149 Forst (Lausitz)
**T +49 3562 98615356/-16**

**Landkreis Teltow-Fläming**

**OFISI YA DAKTARI**
Am Nuthefließ 2
14943 Luckenwalde
**T +49 3371 6083892**

**OFISI YA DAKTARI**
Straße der Jugend 63
14974 Ludwigsfelde
**T +49 3378 803608**

**Landkreis Uckermark**

**GESUNDHEITS- UND VETERINÄRAMT**
Berliner Straße 123
16303 Schwedt/Oder
**T +49 3332 208 137**

**GESUNDHEITS- UND VETERINÄRAMT**
Karl-Marx-Straße 1
17291 Prenzlau
**T +49 3984-703 353**

**Other help offices and HIV test centres:**

**AIDS-HILFE POTSDAM E.V.**
Kastanienallee 27
14471 Potsdam
**T +49 331 95130851**

**AIDS-HILFE LAUSITZ E.V.**
Kulturzentrum
„Bunte Welt"
Thierbacher Str. 21
03048 Cottbus
**T +49 321 21335991**

**RAT & TAT ZENTRUM POTSDAM**
Jägerallee 29
14469 Potsdam
**T +49 331 240190**

This project is financed with the lottery funds of the Ministry for work, social affairs, health and family of the federal state of Brandenburg.

## Ikiwa unahitaji kufanyiwa vipimo au ushauri, mambo yafuatayo ni muhimu kujua:

Vipimo ni vya bila malipo katika vituo vya ushauri vya Brandenburg's na ofisi za afya. **HUHITAJI** maagizo kutoka kwa daktari wako.

**HUHITAJI** kutupa jina lako. Hutatambulika.

Matokeo ya vipimo na ushauri ni vya **SIRI**. Tutazungumza nawe pekee. Hakuna atakayehamishwa kutoka Ujerumani kwa sababu ya hali yake ya VVU.

Ikiwa una maswali yoyote au unadhani kuwa huenda tayari umeambukizwa, tafadhali zungumza na mtu kwenye kituo cha ushauri. Kwa pamoja tunaweza kupata masuluhisho.

## Kujikinga mwenyewe na wengine: vipi?

Mipira ni kinga nzuri sana dhidi ya VVU, maambukizi ya zinaa, na mimba zisizohitajika. Unaweza kupata mipira bila malipo kwenye vituo vya ushauri.

Zungumza kuhusu maambukizo yoyote yanayoweza kuwepo na mwenzako. Mawasiliano ni muhimu sana kwa ajili ya afya ya kila mmoja!

Kwa usaidizi wa:
Deutsche AIDS-Stiftung

## Ziara kwa Daktari

Madaktari wanazingatia sherai za usiri kitaaluma. Huenda wasishiriki taarifa yoyote kukuhusu bila idhini yako (hata si kwa polisi wala mamlaka). Hawaegemei upande wowote na hawaruhusiwi kubagua au kukuhukumu.
Ikiwa hawataheshimu jukumu hili la usiri au wanakubagua, unaweza kupata usaidizi kwenye kituo cha ushauri kuhusu UKIMWI au vituo vya ushauri kwa wakimbizi.
Kumbuka, daktari wako ni mtu muhimu ukiwa na maswali kuhusu afya yako, hata kama huhisi kuwa mgonjwa.

**Ikiwa utaona vigumu** kuzungumza kuhusu VVU/UKIMWI au ngono na mtoa huduma wako wa afya, unaweza kutia alama kisanduku kinachofaa na umpe daktari wako. Anafahamu vyema anavyoweza kusaidia.

**Nimefanya | Ich habe**
- ☐ mapenzi bila kinga (sehemu ya ukeni, sehemu ya haja kubwa) **|** ungeschützten Sex (vaginal, anal)
  - ☐ na mwanamume **|** mit einem Mann
  - ☐ mwanamke **|** mit einer Frau
- ☐ nimegusa damu (kushiriki sindano) **|** Kontakt zu Blut (Spritzenaustausch, Nadel) **gehabt**

**Ilitendeka**
- ☐ chini ya siku 3 zilizopita **|** vor weniger als 3 Tagen
- ☐ siku 4-10 zilizopita **|** vor weniger als 10 Tagen
- ☐ mwezi mmoja uliopita **|** vor 1 Monat
- ☐ miezi miwili iliyopita **|** vor 2 Monaten
- ☐ miezi mitatu au zaidi iliyopita **|** vor 3 Monaten / Es war vor einer längeren Zeit

**Nina**
- ☐ maumivu katika sehemu zangu za siri/ sehemu ya haja kubwa **|** Schmerzen im genitalen/analen Bereich
- ☐ homa **|** Fieber
- ☐ upele **|** Hautausschlag
- ☐ maumivu kwenye mikono/miguu **|** Gliederschmerzen
- ☐ tokwa jasho **|** Nachtschweißausbrüche
- ☐ limfu nodi zimevimba **|** Lymphknotenschwellung

**Ninataka kupimwa**
- ☐ VVU **|** auf HIV
- ☐ maambukuziki mengine ya zinaa **|** auf andere sexuell übertragbare Infektionen **testen lassen.**